JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA RAIS

Menejimenti ya Utumishi
wa Umma,
S.L.P. 2483,
DAR ES SALAAM.

Kumb. Na. C/AC.134/213/01/I/3 — 30 Januari, 2007

## WARAKA WA UTUMISHI NA.1 WA MWAKA 2007 KUHUSU UTARATIBU WA KUPANGIWA NYUMBA VIONGOZI NA WATENDAJI WAKUU SERIKALINI

1.0 **Utangulizi**

1.1 Utaratibu wa kuwapangia nyumba viongozi na watendaji wakuu serikalini ulitolewa kwa Waraka wangu wenye Kumb Na. C/AC/134/23/01/G/69 wa tarehe 30 Januari, 2006 na kufafanuliwa zaidi katika Waraka wenye Kumb. Na. C/AC/134/213/01/21 wa tarehe 21 Machi, 2006. Tangu kutolewa kwa nyaraka hizo kumekuwepo na matatizo ya kiutekelezaji ambayo yanahitaji kurekebishwa. Matatizo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Si watumishi wote wenye stahili walipata au kuuziwa nyumba ya Serikali,

(ii) Maeneo mengine hayana nyumba za Serikali za kuwapatia viongozi na watendaji wenye stahili ya kupatiwa nyumba.

1.2 Kutokana na matatizo haya, Serikali imeamua kuweka utaratibu mbadala wa kuwahudumia viongozi na watendaji

wakuu ambao kwa mujibu wa masharti yao ya kazi, wanastahili kupatiwa nyumba na Serikali ambayo hawatailipia pango.

2.0 **Madhumuni ya Waraka huu**

Madhumuni ya Waraka huu, ni kuweka utaratibu mzuri wa kutoa huduma ya nyumba kwa watumishi wa Serikali waandamizi ambao masharti yao ya kazi ni pamoja na kupatiwa nyumba na Serikali ambayo hawatailipia pango.

**3.0. Uamuzi wa Serikali**

3.1. Watumishi wote wenye stahili ya kupatiwa nyumba na Serikali bila kulipia pango, na ambao hawajapatiwa wala kuuziwa nyumba ya Serikali watalipwa asilimia 30% ya mishahara yao ili waweze kupanga wenyewe nyumba.

3.2 Pamoja na uamuzi huu wa Serikali posho ya asilimia 30% ya mshahara italipwa baada ya uthibitisho wa Katibu Mkuu, Wizara ya Miundombinu kuwa hakuna nyumba ya kumpatia mtumishi anayehusika. Sharti hili litawahusu watumishi walioko Mkoa wa Dar es Salaam.

3.3 Kwa wale wa Mikoani/Wilayani, watatakiwa kupata uthibitisho wa kutokuwepo nyumba kutoka kwa Meneja wa Wakala wa Majengo wa Mkoa husika.

3.4 Watumishi waliouziwa nyumba za Serikali hawatapewa nyumba nyingine wala kulipwa asilimia 30% ya mishahara yao.



3.5 Kutokana na uamuzi huu Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Idara zinazojitegemea na Wakurugenzi Watendaji wa Majiji, Miji, Manispaa, na Wilaya, wahakikishe kuwa kila inapowezekana watumishi ambao kwa mujibu wa barua zao za uteuzi wanastahili kupatiwa nyumba bila kulipia pango, wanapewa kipaumbele katika kugawiwa nyumba zinazoendelea kujengwa na Wakala wa Majengo (Tanzania Building Agency).

**4.0 Watumishi wanaoishi katika nyumba za Taasisi:**

Utaratibu huu hautawahusu watumishi wanaoishi katika nyumba za Taasisi kama vile nyumba za Walimu, Polisi, Magereza na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, ambao wataendelea na utaratibu uliopo.

**5.0 Mwisho**

Waraka unaanza kutumika mara moja.

RUTH H. MOLLEL.
*Katibu Mkuu (Utumishi)*